# Serikali Mtandao

www.ega.go.tz

Toleo Maalum : Machi, 2026



# Kikao Kazi cha 6 cha Serikali Mtandao



## Balozi Dkt. Kusiluka ataja Maeneo 10 Kuimarisha Serikali Mtandao

Ridhiwani atoa tahadhari mashambulio ya kimtandao >>>uk 01

e-GA Yaanika Mikakati Kutekeleza Dira 2050, Yajivunia Mafanikio >>>uk 06

Mapinduzi ya Kidigitali Mahakamani: Hukumu sasa zaandikwa kwa Akili Unde >>>uk 10

Utekelezaji Maazimio Kikao Kazi cha Tano Waleta tija Serikali Mtandao >>>Uk. 14

# WADHAMINI WETU

| Aina ya Udhamini | Jina la Taasisi |
| --- | --- |
| TANZANITE SPONSOR | Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete<br>yas<br>SoftNet Creativity at Work<br>TCDC Together We Build Our Economy<br>Hifadhi za Taifa Tanzania National Parks<br>Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari<br>SOPHOS Defeat Cyberattacks |
| DIAMOND SPONSOR | PPRA Public Procurement Regulatory Authority<br>TTCL Corporation |
| GOLD SPONSOR | NMB Close to you<br>SBT Bukari |
| SILVER SPONSOR | Cra<br>TBC Ukweli na Uhakika<br>CRDB Bank<br>NBC National Bank of Commerce<br>NSSF<br>scancode<br>HESLB Bodi ya Mikopo Investing in the Future<br>Tanzania Airports Authority<br>Computer Centre<br>PSSSF<br>msd medical stores department<br>UCSAF<br>cybergen Training with Excellence |
| BRONZE SPONSOR | TASAC<br>OSHA<br>TADB Tanzania Agricultural Development Bank<br>Watumishi Housing Investments<br>LATRA<br>ISO 9001: 2015<br>TANESCO<br>Tanzania Forest Services Agency<br>WCF Workers Compensation Fund ISO 9001 : 2015 Certified<br>TPA<br>National Internet Data Center<br>TASHICO<br>NHIF<br>NHC<br>PDPC<br>TAWA<br>TMX<br>Unique Academy<br>CAHOOT Technologies Pvt Ltd<br>TISEZA |

# Yaliyomo

**Nukuu ya Mwenyekiti wa Bodi**
**Uk. iV**

**Ujumbe wa Mkurugenzi Mkuu**
Shukrani kwa Washiriki wa Kikao Kazi cha 6 cha Serikali Mtandao **Uk. v**

**Tahariri**
Maazimio ya Kikao Kazi cha 6 cha Serikali Mtandao Msingi Imara wa Serikali ya Kidijitali **Uk. vi**

**Habari**
Ridhiwani atoa tahadhari mashambulio ya kimtandao **Uk. 01**

**Habari**
Dkt. Kusiluka ataja Maeneo 10 Kuimarisha Serikali Mtandao **Uk. 04**

**Habari**
e-GA Yaanika Mikakati Kutekeleza Dira 2050, Yajivunia Mafanikio **Uk. 06**

**Habari**
Wadau Waipongeza e-GA Kuleta Mageuzi ya Kidigitali Serikalini **Uk. 08**

**Habari**
Mapinduzi ya Kidigitali Mahakamani: Hukumu sasa Zaandikwa kwa Akili Unde **Uk. 10**

**Habari**
e-GA Yatoa Tuzo kwa Taasisi Kinara Serikali Mtandao **Uk. 12**

**Habari**
Utekelezaji Maazimio Kikao Kazi cha Tano Waleta tija Serikali Mtandao **Uk. 14**

Matukio katika picha **Uk. 16**



Mafanikio ya ajenda ya Serikali Mtandao hayawezi kupatikana kupitia taasisi moja pekee; yanahitaji mshikamano, ushirikiano wa karibu wa wadau wote, na uwajibikaji wa pamoja kuanzia hatua za upangaji, utekelezaji hadi ufuatiliaji wa miradi ya TEHAMA katika taasisi za umma.

**Dkt. Mussa Kissaka**
**Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi e-GA**

**Tarehe 17 Februari, 2026 AICC**

## BODI YA UHARIRI

| | |
|---|---|
| **Mwenyekiti** | Eng. Benedict B. Ndomba<br>Mkurugenzi Mkuu |
| **Mhariri** | Subira J. Kaswaga<br>Meneja Mawasiliano |
| **Wajumbe** | SACP. Hamis Ali<br>Mkaguzi mkuu wa Ndani<br><br>SACP. Rafael Ruthahiwa<br>Meneja wa Huduma za Sheria<br><br>Long'ida Oltetiai<br>Meneja wa Huduma kwa wateja na Takwimu |
| **Wapiga Picha** | Benchine Bago<br>Afisa Habari<br><br>Mussa Enock<br>Afisa Habari |
| **Msanifu Kurasa** | Edger Msamba<br>Afisa TEHAMA |

# Shukrani kwa Washiriki wa Kikao Kazi cha 6 cha Serikali Mtandao



**Mhandisi Benedict Ndomba**
**Mkurugenzi Mkuu e-GA**

Kwa niaba ya uongozi na wafanyakazi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa washiriki wote waliohudhuria na kuchangia kwa namna mbalimbali katika mafanikio ya Kikao Kazi cha 6 cha Serikali Mtandao, kilichofanyika Februari 17 – 19, 2026 jijini Arusha. Mawazo yenu ya kujenga pamoja na uzoefu mliochangia, umeongeza thamani kubwa katika juhudi zetu za kuendeleza na kuimarisha utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao nchini.

Kikao kazi hiki kimekuwa jukwaa muhimu la kubadilishana uzoefu, kujadili changamoto na fursa, pamoja na kuweka mikakati madhubuti ya kuboresha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za umma. Kupitia mijadala na mapendekezo yaliyotolewa, tunaendelea kujenga msingi imara wa kuhakikisha kuwa huduma za serikali zinakuwa bora zaidi, zenye ufanisi, uwazi na zinazowafikia wananchi kwa urahisi zaidi.

Mamlaka inaendelea kujipanga kuimarisha mifumo ya kidijitali Serikalini, kuongeza ushirikiano kati ya taasisi za umma na binafsi, na kuhakikisha kuwa sheria na miongozo ya Serikali Mtandao inatekelezwa kwa ufanisi. Aidha, tutaendelea kuwekeza katika ubunifu, kujenga uwezo wa rasilimali watu, na kuboresha miundombinu ya TEHAMA ili kuendana na mahitaji ya sasa na ya baadaye ya huduma za serikali.

Napenda pia kutoa shukrani za pekee kwa wadhamini wetu 50 ambao wamechangia kufanikisha kikao kazi hiki. Mchango wenu umeonyesha dhamira ya pamoja ya kushirikiana na serikali katika kuimarisha matumizi ya teknolojia kwa maendeleo ya taifa. Naomba kuwatambua wadhamini wakuu kumi na tatu (13) ambao ni; **Taasisi ya Moyo ya Jakata Kikwete (JKCI), Kampuni ya Yas, SOFTNET, SOPHOS, Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Shirika la Mendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Bodi ya Sukari, Kampuni ya Simu za Mkononi VODACOM na Benki ya NMB.**

Kwa mara nyingine tena, nawapongeza washiriki wote kwa kujitoa kwenu na ushiriki wenu wenye tija. Tunaamini kuwa mawazo na maazimio yaliyofikiwa katika kikao hiki yatakuwa chachu ya kuendelea kuboresha utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao na kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi.

Asanteni sana kwa ushirikiano wenu, na tunatarajia kuendelea kushirikiana nanyi katika hatua zinazofuata za utekelezaji wa ajenda ya Serikali Mtandao.

# Maazimio ya Kikao Kazi cha 6 cha Serikali Mtandao Msingi Imara wa Serikali ya Kidijitali



**Bi. Subira Kaswaga**
**Meneja Mawasiliano e-GA**

Kikao Kazi cha Sita cha Serikali Mtandao kimehitimishwa kwa maazimio muhimu yanayolenga kuimarisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika taasisi za umma. Maazimio haya yanaweka mkazo katika ushirikiano, uwajibikaji, usalama wa mifumo pamoja na matumizi bora ya rasilimali za TEHAMA ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Moja ya maeneo yaliyopewa kipaumbele ni kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi za umma, taasisi za elimu ya juu na sekta binafsi. Ushirikiano huu unatarajiwa kusaidia kuhakikisha matokeo ya tafiti na ubunifu katika TEHAMA yanatumika kwa vitendo katika kuboresha huduma za serikali na kuongeza ufanisi katika utendaji wa taasisi za umma.

Aidha, kikao hicho kimesisitiza umuhimu wa usimamizi madhubuti wa mikataba ya ununuzi wa rasilimali za TEHAMA. Usimamizi sahihi wa mikataba utasaidia kuhakikisha kuwa uwekezaji unaofanywa na Serikali katika teknolojia unaleta thamani halisi na tija kwa taifa, huku ukipunguza hatari ya matumizi yasiyo na ufanisi wa rasilimali za umma.

Katika zama za ongezeko la matumizi ya mifumo ya kidijitali, usalama wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA umepewa uzito mkubwa. Taasisi za umma zimetakiwa kuzingatia kikamilifu miongozo ya usimamizi wa usalama wa Serikali Mtandao, pamoja na kuwajengea uwezo watumiaji na maafisa TEHAMA kupitia mafunzo ya mara kwa mara ili kukabiliana na changamoto za usalama wa mifumo.

Maazimio hayo pia yanasisitiza umuhimu wa taasisi za umma kuimarisha mifumo ya usimamizi wa TEHAMA ndani ya taasisi zao, ikiwemo kuhakikisha Kamati za Kitaasisi za Uendeshaji wa TEHAMA zinafanya vikao kwa wakati na kuwasilisha taarifa zake kwa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo.

Sambamba na hilo, taasisi za umma zimetakiwa kuchukua hatua za haraka kufanyia kazi ushauri na mapendekezo yanayotolewa kuhusu vihatarishi au mapungufu katika mifumo ya TEHAMA kutoka taasisi za usimamizi na ukaguzi kama vile e-GA, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali (IAG) na mamlaka nyingine za serikali. Hatua hii inalenga kuimarisha uwajibikaji na kupunguza hatari zinazoweza kuathiri mifumo ya serikali.

Vilevile, kikao kimehimiza taasisi za umma kufanya tathmini na kuainisha rasilimali zote za TEHAMA zilizopo, ili kuhakikisha zinatumika kwa ufanisi zaidi na kuendelea kuongeza thamani katika utoaji wa huduma za serikali. Hatua hii itasaidia kuimarisha matumizi bora ya rasilimali zilizopo na kuepuka matumizi yasiyo ya lazima ya fedha za umma.

Hatimaye, kikao hicho kimesisitiza umuhimu wa kuwajengea uwezo Maafisa TEHAMA mara kwa mara ili waweze kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia duniani. Uwekezaji katika rasilimali watu ni nguzo muhimu katika kuhakikisha mifumo ya Serikali Mtandao inaendeshwa kwa ufanisi na kuendelea kuboresha huduma kwa wananchi.

Kwa ujumla, maazimio ya Kikao Kazi cha Sita cha Serikali Mtandao yanaweka msingi imara wa kuendelea kuijenga Serikali ya Kidijitali yenye ufanisi, usalama na uwazi zaidi. Utekelezaji wa maazimio haya unahitaji dhamira ya pamoja ya taasisi zote za umma ili kuhakikisha teknolojia inatumika kikamilifu katika kuimarisha utendaji wa serikali na kutoa huduma bora kwa wananchi.



# Waziri Ridhiwani atoa tahadhari mashambulio ya kimtandao

Na. Catherine Peter | Afisa Habari Mwandamizi

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete(Mb), amewataka wadau wa Serikali Mtandao kuendelea kuchukua tahadhari za kulinda mifumo ya Serikali ili kuepukana na mashambulio ya kimtandao.

Waziri Ridhiwani pia amesisitiza umuhimu wa kuwajengea uwezo wataalamu wa TEHAMA ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya Teknolojia.

Akifunga Kikao Kazi cha Sita cha Serikali Mtandao kilichofanyika kwa siku tatu jijini Arusha kuanzia Februari 17-19, 2026 kilichoratibiwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Waziri Ridhiwani amesema ni lazima taasisi za umma ziweke kipaumbele katika usalama wa mifumo yao na kuwekeza zaidi katika mafunzo ya wataalamu.

Kikao hicho chenye kauli mbiu 'Kuboresha Utendaji kazi wa Serikali kwa Kuimarisha Utoaji wa Huduma za Umma kupitia Mifumo Salama na Jumuishi ya Serikali Mtandao', kilihudhuriwa na wadau zaidi ya 1400 kutoka taasisi mbalimbali.

**"Moja ya changamoto kubwa tunayopata ni matishio ya mashambulio ya kimtandao, niwaombe muendelee kulichukulia jambo hili kwa umakini na kuwapa wataalamu wetu nafasi ya kuendelea kujifunza ili wawe mahiri zaidi".**

Ametahadharisha kuwa sekta ya TEHAMA hubadilika kwa kasi kubwa, hivyo bila uwekezaji katika maarifa mapya, wataalamu wanaweza kubaki nyuma na kuiweka Serikali katika hatari ya kiusalama.

Akitoa mfano wa kimataifa, Waziri Ridhiwani amesema baadhi ya nchi zimeanzisha mashindano ya kupima uimara wa mifumo yao kwa kuwahusisha wataalamu wa usalama wa mitandao (hackers) ili kubaini mianya ya kiusalama na kuifanyia maboresho kabla ya mifumo kushambuliwa.

"Nimeona baadhi ya nchi kama Indonesia, Dubai kunakuwa hata na mashindano ya mtu anatengeneza mfumo halafu anauweka hadharani na kuwakaribisha vijana ili wajaribu usalama wa mfumo huo, vijana hao wanaitwa 'hackers', wanajaribu kupenya kuona mfumo upo katika usalama gani na kupitia njia hii, wale wanaotengeneza mifumo wanapata nafasi ya kujua zile njia zinazohatarisha mfumo na kuuweka katika hatari," amesema.

"Kumekuwa na changamoto kubwa bado kuna watumishi wa umma wanaendelea kutumia mitandao binafsi kurusha taarifa rasmi za Serikali, nataka kuwahakikishieni watumishi wenzangu wa umma tunachokifanya ni jambo la hatari sana. Serikali kupitia e-GA imetengeneza mfumo rasmi wa mawasiliano ambayo inaturuhusu sisi watumishi wa umma kutuma taarifa na kubadilishana taarifa katika mfumo ulio salama sana," amesema

"e-GA na washiriki mnayo kazi ya kuendelea kuelimisha umma hasa watumishi wa umma na Serikali juu ya jinsi ambavyo mifumo ya kidigitali imesaidia kwa namna moja au nyingine kutatua kero mbalimbali katika jamii yetu, tena kwa kutumia muda mfupi sana."



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Ridhiwani Kikwete(Mb) akizungumza wakati wa kufunga kikao kazi cha 6 cha Serikali Mtandao Jijini Arusha.*

Naye, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Utawala, Katiba na Sheria, Dkt. Damas Ndumbaro amesema “Kwa dunia ya leo hatuwezi kusonga mbele bila Serikali Mtandao. Suala la TEHAMA limechukua nafasi yake katika maisha na kwa Tanzania tumepata mafanikio kuliko nchi nyingi za Afrika na yanatokana na kazi nzuri iliyofanywa na Serikali inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.”

Amesema Bunge na Kamati hiyo inatambua mafanikio hayo ya kupeleka huduma kwa umma na wananchi wamerahisishiwa kufanya malipo kwa ‘Control Number’ na kwamba hiyo ni kazi iliyofanywa na e-GA, sambamba na kuunganisha mifumo mbalimbali Serikalini.

**“Sisi Bunge tupo tayari kushirikiana na Wizara kuhakikisha kwamba changamoto zinazojitokeza kwenye Mifumo zinapatiwa ufumbuzi, hasa zile zinazogusa Sera, Sheria pamoja na bajeti. Bunge pia ni mnufaika wa Serikali Mtandao, tangu Bunge la 12 hakuna makaratasi kwenye meza za Wabunge, kazi hii nzuri imefanywa na e-GA kwa kushirikiana na Bunge. Jambo hili zuri liende kwa taasisi zote za Serikali ili tuokoe muda, fedha na mwananchi apate huduma popote alipo,”** amesema.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa e-GA, Mhandisi Benedict Ndomba, alisema kikao kazi hicho kimetumika kama jukwaa muhimu la kutafakari na kujadili Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050 katika eneo la Serikali Mandao inayolenga kuijenga Serikali itakayokuwa ya kidigitali na inayotumia mifumo jumuishi na salama.

“Lengo ni kuhakikisha serikali Mtandao inakuwa nyenzo wezeshi katika kukuza uchumi wa kidigitali, nguzo ya uwajibikaji na mapambano dhidi ya rushwa, kichocheo cha ubunifu na matumizi ya teknolojia za kisasa,



*Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Mhandisi Benedict Ndomba akitoa neno la ukaribisho wakati wa kikao kazi cha 6 cha Serikali Mtandao*



*Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Utawala, Katiba na Sheria, Dkt. Damas Ndumbaro akizungumza wakati wa kikao kazi cha 6 cha Serikali Mtandao*

na msingi katika utoaji wa huduma bora jumuishi na zinazopatikana wakati wote, kukuza vipaji na kutengeneza ajira kwa vijana wabunifu katika eneo la Serikali Mtandao,” amesema.

Amebainisha kuwa, Mamlaka ya Serikali Mtandao itaendelea kushirikiana kwa karibu na wadau wote wa Serikali Mtandao kuhakikisha kuwa, Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 inatafsiriwa katika mipango ya utekelezaji wa miradi ya TEHAMA Serikalini ili kuleta tija kwa maendeleo ya taifa.




# Dkt.Kusiluka ataja Maeneo 10 Kuimarisha Serikali Mtandao

Na. Queenter Mawinda | Afisa Habari Mwandamizi

Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Dkt. Moses Kusiluka, ametaja maeneo 10 ya kuzingatia ili kuimarisha utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao zitakazo boresha zaidi utendaji kazi katika taasisi za umma na utoaji wa huduma kwa wananchi.

Dkt Kusiluka amesema hayo wakati akifungua Kikao Kazi cha Sita cha Serikali Mtandao Februari 17, 2026 kilichoandaliwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) jijini Arusha.

Dkt. Kusiluka amesema, mafanikio ya utekelezaji wa Dira ya Maendeleo 2050 yanategemea kwa kiasi kikubwa uwekezaji na usimamizi madhubuti wa TEHAMA.

***Maeneo ya Kuzingatia***

Alitaja maeneo hayo kuwa ni Matumizi salama, jumuishi na yenye tija ya TEHAMA; Kuzingatia Sheria ya Serikali Mtandao ya Mwaka 2019; Kuendeleza ubunifu wa ndani; Kuwekeza katika mafunzo endelevu kwa watumishi; Kudhibiti matishio ya usalama mtandaoni; Kubiasharisha bunifu za kiteknolojia; Kuimarisha usimamizi wa miradi ya TEHAMA Serikalini; Mifumo ya TEHAMA ya Serikali kusomana; Kulinda taarifa binafsi na rasilimali za taifa pamoja na Kushirikiana na taasisi za elimu ya juu katika tafiti na ubunifu.

Alisisitiza kuwa, wataalamu wa TEHAMA wanapaswa kuhakikisha mifumo wanayobuni na kuisimamia inalinda maslahi ya taifa na usalama wa nchi. Aidha, amesema Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imeweka TEHAMA kuwa kipaumbele cha kitaifa.

"Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan inaipa umuhimu teknolojia. Rais anaishi kwenye TEHAMA na anatumia TEHAMA, kwa hiyo TEHAMA ni kipaumbele cha Serikali," alisema.

Dkt. Kusiluka aliipongeza Bodi na uongozi wa e-GA kwa hatua kubwa iliyofikiwa katika kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi kupitia mifumo ya kidigitali.

Alisema,Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizopiga hatua kubwa duniani katika matumizi ya TEHAMA kwenye utekelezaji wa shughuli za Serikali, huku akibainisha kuwa mifumo mingi inayotumika Serikalini imebuniwa na watumishi wa umma wenyewe.

**"Mwanzo watumishi wetu hawakuaminika, lakini wachache walisimama kidete kudhihirisha kwamba tunaweza. Yanayowezekana huko kwa wenzetu kwa nini kwetu yasiwezekane?"** alisema.

Aliongeza kuwa, wataalamu wa TEHAMA wa Tanzania wana uwezo wa kushindana




*Mhe. Balozi Dkt. Mosses Kusiluka akihutubia washiriki wa kikao kazi cha 6 cha Serikali Mtandao wakati wa ufunguzi wa kikao kazi hicho.*

kimataifa na baadhi yao wamefanya vizuri katika taasisi kubwa duniani pamoja na mashindano ya kimataifa wakiwa vyuoni.

Akizungumzia changamoto za usalama mtandaoni, alionya juu ya matumizi mabaya ya teknolojia ikiwemo uhalifu wa kimtandao na upotoshaji wa taarifa, na kuhimiza usimamizi makini wa teknolojia zinazochipukia, kama Akili Unde (AI).

**“Nitoe wito kwenu kuhakikisha mnatumia au kusimamia teknolojia hii ili ituletee maendeleo badala ya uhalifu au uharibifu... ni muhimu kulinda mila, desturi na mshikamano wa Taifa,”** alisema.

Alizitaka Taasisi za Umma kuhakikisha mifumo yao inasomana ili kuepuka urudufu na upotevu wa rasilimali, akibainisha kuwa jitihada za e-GA zimepunguza kwa kiasi kikubwa changamoto hiyo na kuwezesha ubadilishanaji wa taarifa Serikalini kupitia mifumo ya TEHAMA.

Kadhalika, amezikumbusha taasisi kuzingatia kikamilifu Sheria ya Serikali Mtandao ya Mwaka 2019 pamoja na Kanuni na Miongozo yake, na kuonya dhidi ya mikataba isiyoendana na kukidhi mabadiliko ya teknolojia.

Amesisitiza umuhimu wa watumishi kupata mafunzo ya mara kwa mara ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya kiteknolojia, ili kuwa mifumo ya TEHAMA iliyothabiti inayojibu matatizo yaliyopo, pamoja na kuepuka hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) zinazotokana na udhaifu katika mifumo inayotumika.

“Kikao kazi hiki kinapaswa kuwa jukwaa la majadiliano ya wazi, kubadilishana uzoefu na kuweka maazimio yanayotekelezeka, ili kufikia lengo la Dira ya Maendeleo 2050 la kuhakikisha zaidi ya asilimia 80 ya huduma za Serikali zinapatikana kidigitali kwa usalama, uwazi na gharama nafuu,”amesema.

Naye, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Bw. Xavier Daudi, amesema kwa kuwa serikali Mtandao ni nyenzo muhimu katika kuboresha utoaji wa huduma kwa umma, Serikali itaendelea kuimarisha Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa kutenga rasilimali zaidi.

Awali, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa e-GA, Dkt. Mussa Kissaka, alisema licha ya jukumu la kisheria la e-GA la Kuratibu, Kuendeleza na Kusimamia jitihada za Serikali Mtandao, mafanikio ya jitihada hizi yanahitaji mshikamano na ushirikiano wa karibu wa wadau wote na kwamba majadiliano ya kikao kazi hicho yatasaidia kuboresha huduma za Serikali Mtandao.



Mhandisi Benedict Ndomba
Mkurugenzi Mkuu e-GA

# e-GA Yaanika Mikakati Kutekeleza Dira 2050, Yajivunia Mafanikio

Na. Benchine Bago | Afisa Habari

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) imeanika mikakati yake ya kutekeleza malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050, yanayolenga asilimia 80 ya huduma za Serikali zipatikane kupitia mifumo ya kidigitali iliyo salama na jumuishi.

Miongoni mwa mikakati hiyo ni kuimarisha usimamizi wa mtandao wa mawasiliano ya Serikali pamoja na mifumo ya TEHAMA, ili kupunguza urudufu wa mifumo na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za umma.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Mhandisi Benedict Ndomba ameyasema hayo Februari 17, 2026 katika Kikao Kazi cha Sita cha Serikali Mtandao kilichofanyika Februari 17, 2026 jijini Arusha.

Kauli mbiu ya Kikao kazi hicho kilichohudhuriwa na wadau zaidi ya 1400 ni *"Kuboresha utendaji kazi wa Serikali kwa Kuimarisha Utoaji wa Huduma za Umma Kupitia Mifumo Salama na Jumuishi ya Serikali Mtandao".*

Mhandisi Ndomba amesema, hatua hizo zinawezesha Serikali kurahisisha ubadilishanaji wa taarifa kati ya taasisi mbalimbali za umma, jambo linaloongeza kasi ya utoaji huduma na kupunguza gharama za uendeshaji wa mifumo ya TEHAMA Serikalini.

Ameeleza kuwa, utekelezaji wa mikakati hiyo unaendana pia na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2025, inayolenga kuhakikisha zaidi ya asilimia 50 ya huduma za Serikali zinapatikana kidigitali ifikapo mwaka 2030.

Kwa upande wa mafanikio ya kimataifa, amesema utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao umeiwezesha Tanzania kutambulika katika majukwaa mbalimbali, ikiwemo kupata tuzo za ubunifu katika huduma za umma kutoka Umoja wa Mataifa Mwaka 2024 na 2025 kupata tuzo ya 'World Summit on the Information Society - WSIS'kupitia mfumo wa e-Mrejesho toleo la pili, uliosaidia kuimarisha ushiriki wa wananchi katika utoaji wa maoni na maboresho ya huduma za Serikali.

Aidha, amesema Ripoti ya mwaka 2025 ya Benki ya Dunia kuhusu ukomavu wa matumizi ya teknolojia jumuishi katika utoaji wa huduma za Serikali, imeiorodhesha Tanzania katika kundi A la nchi zenye ukomavu wa juu wa matumizi ya TEHAMA, hatua inayoonesha mafanikio ya mageuzi ya kidigitali Serikalini.

"Mwaka 2022 Tanzania pia ilitajwa kuwa miongoni mwa nchi zinazofanya vizuri zaidi katika eneo hilo na kushika nafasi ya pili barani Afrika. Nimshukuru Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jitihada zake za kuwezesha sekta ya TEHAMA na mageuzi ya kidigitali, sambamba na kuiwezesha Mamlaka kutekeleza majukumu yake," amesema.

**"Kauli mbiu ya mwaka huu inaakisi dhamira ya Serikali ya kutumia mifumo ya kidigitali iliyo salama na jumuishi ili kuongeza tija, ufanisi na uwajibikaji katika utendaji kazi pamoja na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi."**
Mhandisi Benedict Ndimba
Mkurugenzi Mkuu e-GA.

Hata hivyo, ametaja changamoto zinazokabili utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao kuwa ni pamoja na upungufu wa wataalam wabobezi wa TEHAMA, mabadiliko ya haraka ya teknolojia yanayohitaji mafunzo ya mara kwa mara, kwa watumishi, pamoja na umuhimu wa taasisi kuimarisha usimamizi wa miradi ya TEHAMA ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mhandisi Ndomba amesema jumla ya wadhamini **50**, wamedhamini kikao kazi hicho, ambapo kati yao 13 ndio wadhamini wakuu, ambao ni **Taasisi ya Moyo ya Jakata Kikwete (JKCI), Kampuni ya Yas, SOFTNET, SOPHOS, Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Shirika la Mendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Bodi ya Sukari, Kampuni ya Simu za Mkononi VODACOM na Benki ya NMB.**





Dkt. Benson O. Ndiege
Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania

# Wadau Waipongeza e-GA Kuleta Mageuzi ya Kidigitali Serikalini

Na. Mussa Enock | Afisa Habari

Wadau wameipongeza Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa kuendelea kuimarisha mifumo ya TEHAMA Serikalini na kuongeza ufanisi wa utoaji huduma kwa wananchi.

Wakizungumza katika kikao kazi cha sita cha Serikali Mtandao kilichofanyika jijini Arusha, wadau hao wamesema juhudi za e-GA zimekuwa chachu ya kuharakisha mageuzi ya kidigitali Serikalini na kuweka msingi imara wa utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 kupitia huduma jumuishi, salama na zinazowafikia wananchi popote walipo.

### Kampuni ya Yas

Mkuu wa Miradi ya Kimkakati kampuni ya Mawasiliano ya YAS, William Mpinga, amesema kampuni hiyo inaunga mkono jitihada za Serikali katika kujenga Serikali ya kidijitali, kwa kuimarisha mawasiliano na huduma za fedha kidigitali.

Amesema, dhamira ya Yas ni kuwa mshirika sahihi wa Serikali katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma rahisi na jumuishi, akibainisha kuwa kampuni hiyo imewekeza zaidi ya shilingi trilioni moja kuboresha miundombinu ya mitandao mijini na vijijini.

**"Yas itaendelea kuwa mshirika madhubuti wa Serikali katika kujenga taifa lenye mifumo imara na huduma jumuishi kwa kushirikiana na e-GA na taasisi nyingine".**

**Mr William Mpinga**
Mkuu wa Miradi ya Kimkakati kampuni ya Mawasiliano ya YAS

Ameongeza kuwa Yas kwa sasa inaendesha mtandao mkubwa wa 5G nchini unaofikia zaidi ya asilimia 95 ya wananchi na kuhudumia zaidi ya wateja milioni 29. Kupitia ushirikiano na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), kampuni hiyo inaendelea kupanua huduma ili kuhakikisha Watanzania wote wananufaika na fursa za kidigitali.

### Kampuni ya SoftNet

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa SoftNet, Nuru Yakubu Othman amesema kikao kazi hicho kimekuwa jukwaa muhimu la kukutana na wadau wa TEHAMA, huku akibainisha kuwa kampuni hiyo imeshiriki mikutano yote tangu ilipoanzishwa.

Amesema, SoftNet imeendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali kutekeleza miradi ya kidigitali na sasa inatoa huduma nchi nzima, ikijikita katika miundombinu ya kidigitali, usalama mtandaoni, utawala wa mifumo pamoja na huduma zinazohusisha Akili Unde (AI).

Aidha, ameeleza kuwa kampuni hiyo inaendelea kuimarisha kitengo cha mafunzo ili kuwajengea uwezo wananchi na watumishi wa umma katika matumizi sahihi ya mifumo ya kidigitali.

### SOPHOS

Naye, Mwakilishi wa kampuni ya SOPHOS, Rajkumar Popat ameeleza kuwa Tanzania inapiga hatua kubwa katika mageuzi ya kidigitali, jambo linaloongeza umuhimu wa kuimarisha usalama wa mtandao.

Amesema kadri huduma za Serikali zinavyozidi kuhamia mtandaoni, ndivyo haja ya kujifunza na kujikinga dhidi ya matishio ya usalama mtandaoni inavyoongezeka, akisisitiza kuwa usalama wa mtandao ni muhimu katika kulinda wananchi, taswira ya nchi na uchumi wa taifa.

Ameahidi kuendelea kushirikiana na Serikali na e-GA katika safari ya kulifanya taifa kuwa salama kidigitali.

### TCDC

Mrajisi wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dkt. Benson Ndiege, amesema kwenda kidigitali ni hatua muhimu katika kuimarisha maendeleo ya ushirika nchini.

Amesema mifumo ya kidigitali imewezesha upatikanaji wa takwimu sahihi na kusaidia kudhibiti changamoto za ubadhirifu na upotevu wa mali zilizowahi kujitokeza katika vyama vya ushirika

**wa kushirikiana na e-GA, tume hiyo imeanzisha Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU), ambapo hadi sasa vyama 6,466 vimesajiliwa na vinatumia mfumo huo katika shughuli zao za kila siku**

Dkt. Ndiege amewahimiza wadau wa TEHAMA kuendelea kushirikiana na vyama vya ushirika kwa kutoa mifumo, vifaa na ushauri wa kitaalamu ili kuongeza ufanisi na tija katika sekta hiyo muhimu ya uchumi.



# Mapinduzi ya Kidigitali Mahakamani: Hukumu sasa Zaandikwa kwa Akili Unde

Na. Catherine Peter | Afisa Habari Mwandamizi

**Katika hatua inayotajwa kama mapinduzi ya kihistoria kwenye utoaji wa haki, Mahakama ya Tanzania imeanza kutumia Akili Unde (AI) katika uandishi wa hukumu, hatua inayorahisisha, kuharakisha na kuongeza uwazi wa mashauri huku ikiimarisha imani ya wananchi kwa mhimili huo wa dola.**

Akizungumza katika Kikao Kazi cha sita cha Serikali Mtandao kilichofanyika jijini Arusha Februari 17 hadi 19, 2026, Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Prof. Elisante Ole Gabriel, amesema hukumu sasa zinaandikwa kwa kutumia teknolojia za kisasa.

"Kwa sasa hukumu zinaendeshwa kwa takwimu (data-driven). Tulitambua kuwa tunahitaji nguvu ya AI na matokeo yake yamekuwa ya kushangaza," amesema Profesa Gabriel wakati akiwasilisha mada yake mbele ya Viongozi wa Taasisi za Umma, wataalamu wa TEHAMA na wadau kutoka ndani na nje ya nchi.

Ameeleza kuwa, Mwaka 2024 Mahakama ilianza majaribio ya Mfumo wa Kunukuu na Kutafsiri kwa njia ya sauti (Transcription and Translation Software - TTS), ambao tayari umejaribiwa katika kanda 11 za Mahakama nchini.

Kwa mujibu wake, mfumo huo umebadili kwa kiasi kikubwa namna hukumu zinavyoandikwa na kupunguza muda unaotumika.

"Zamani Jaji alikuwa anatumia muda mrefu kuandika hukumu yenye kurasa 200. Sasa Jaji anazungumza na mfumo unaandika moja kwa moja kwa Kiswahili au Kiingereza. Hii imeongeza ufanisi na pia inalinda afya na ustawi wa Majaji," amefafanua.

Profesa Gabriel amesema, lengo kuu la matumizi ya AI na TEHAMA ni kuhakikisha upatikanaji wa haki kwa wakati, kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa mashauri na kuimarisha uwazi katika utoaji wa huduma za Mahakama.

Amebainisha kuwa, mageuzi hayo tayari yameanza kuzaa matunda kwa kuongeza imani ya wananchi kwa Mahakama. "Mwaka 2019 kiwango cha imani ya umma kwa Mahakama kilikuwa asilimia 70, lakini kufikia Mwaka 2023 kimeongezeka hadi asilimia 88," amesema.

Mbali na uandishi wa hukumu, Mahakama imeimarisha pia ushirikiano wa kubadilishana taarifa na taasisi muhimu za umma zikiwemo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Wakala wa Usajili wa Leseni (BRELA), hatua inayorahisisha uratibu na utoaji wa huduma.

Akitolea mfano wa upana wa huduma za Mahakama nchini, alisema kwa kuwa Tanzania ina zaidi ya kata 3,956, matumizi ya teknolojia yanaisaidia Mahakama kuwafikia wananchi kwa ufanisi zaidi katika maeneo yote ya nchi bila kujali umbali wa



*Katibu Tume ya Utumishi wa Mahakama Profesa Elisante Ole Gabriel akielezea jinsi Mahakama inavyotumia TEHAMA na teknolojia ya Akili Unde katika kuendesha shughuli za mahakama.*

kijiografia.

Amesisitiza kuwa mafanikio hayo hayawezi kupatikana bila uongozi imara na matumizi sahihi ya rasilimali.

**"Kuwa na fedha ni jambo moja, kuzitumia kwa ufanisi ni jambo lingine," amesisitiza, akiwataka watendaji wakuu kuwekeza kwa nguvu katika wataalamu wa TEHAMA kama mtaji wa kibinadamu, si rasilimali watu tu.**

Kwa mujibu wa takwimu alizowasilisha, Mahakama kwa sasa inatekeleza zaidi ya programu 17, ambapo takribani asilimia 90 zinahusu maendeleo ya TEHAMA na rasilimali watu.

Miongoni mwa mageuzi makubwa yanayoendelea ni utekelezaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Mashauri (Electronic Case Management System) unaolenga kuondoa matumizi ya mafaili ya karatasi na kuweka mfumo wa kidigitali.

**"Sasa mwananchi anaweza kufungua kesi akiwa popote alipo, kufuatilia ni hakimu gani anashughulikia shauri lake na kunufaika na uwazi zaidi," amesema.**


Aidha, amebainisha kuwa TEHAMA imeongeza urahisi kwa mashahidi kutoa ushahidi kwa njia ya mtandao bila kulazimika kusafiri umbali mrefu.

"Nani angeamini kuwa mtu aliyeko Canada anaweza kutoa ushahidi bila kuja Tanzania?" amehoji na kusisitiza kuwa mageuzi ya kidigitali ndani ya Mahakama lazima yaongozwe na uongozi thabiti ili kuhakikisha mabadiliko hayo yanakuwa endelevu na yenye tija kwa kizazi cha sasa na kijacho.

Kikao kazi hicho kimekutanisha viongozi wakuu wa taasisi mbalimbali za umma, wataalamu wa TEHAMA na wadau wa maendeleo kutoka nchi tofauti, ambapo mada mbalimbali ziliwasilishwa zikionesha namna Tanzania inavyoendelea kuwekeza katika teknolojia ili kuongeza uwazi, uwajibikaji na ufanisi katika utumishi wa umma.



# e-GA Yatoa Tuzo kwa Taasisi Kinara Serikali Mtandao




*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb) pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Mhandisi. Benect Ndomba wakitazama video ya kutangaza washindi wa tuzo mbalimbali wakati wa kikao kazi cha 6 cha Serikali Mtandao.*

Na. Benchine Bago| Afisa Habari

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) imetoa tuzo kwa taasisi za umma zilizofanya vizuri katika maeneo mbalimbali ya utekelezaji wa Sheria ya Serikali Mtandao.

Maeneo hayo ni Taasisi zilizofanya vizuri katika uzingatiaji wa sheria ya Serikali Mtandao, Viwango na Miongozo, Taasisi kinara katika kuunganisha na kubadilishana taarifa kupitia Mfumo wa Kubadilishana Taarifa Serikalini (GoVESB) na Taasisi hodari kwenye matumizi ya TEHAMA katika kuwashirikisha wananchi.

Akikabidhi tuzo hizo katika kikao kazi cha sita cha Serikali Mtandao Februari 19, 2026 jijini Arusha, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb), amesema tuzo hizo zisiwe heshima kwa washindi hao bali pia iwe chachu ya uwajibikaji na uzingatiaji wa misingi ya Sheria ya serikali Mtandao katika taasisi za umma.

**"Tuzo hizi zinalenga kukuza utamaduni wa uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Viwango vya Serikali Mtandao, kuhamasisha ubunifu na matumizi bora ya rasilimali za umma na kupunguza urudufu wa miradi ya TEHAMA Serikalini na kuhakikisha mifumo ya TEHAMA inachangia kikamilifu katika utoaji wa huduma kwa wananchi wetu,"**

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa e-GA, Mhandisi Benedict Ndomba, Mamlaka imeandaa tuzo kwa taasisi zilizofanya vizuri katika uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao, katika ujenzi, uendelezaji, uendeshaji na usimamizi wa miradi ya TEHAMA Serikalini.

Amesema, Tuzo zinalenga kutambua na kuthamini jitihada za taasisi za umma zilizotekeleza miradi ya TEHAMA kwa weledi, uwajibikaji na kwa kuzingatia misingi ya Serikali Mtandao ili kuwa mfano na kutoa hamasa kwa taasisi nyingine.

"Umuhimu wa tuzo hizi ni pamoja na kukuza utamaduni wa uzingatiaji wa Sheria, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao, kuhamasisha ubunifu

na ubora katika utekelezaji wa miradi ya TEHAMA, kuhamasisha taasisi nyingine kuzingatia kikamilifu sheria, kanuni, taratibu, miongozo iliyowekwa na pia kuhakikisha mifumo ya TEHAMA inakuwa salama, endelevu, jumuishi na inayotoa thamani halisi kwa taifa," amesema.

Katika kundi la kwanza la taasisi zilizofanya vizuri katika uzingatiaji wa Sheria ya Serikali Mtandao, Viwango na miongozo, kipengele cha kwanza taasisi katika ngazi ya nne ya ukomavu wa TEHAMA Serikalini, mshindi wa kwanza ni Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), mshindi wa pili ni Chuo Kishiriki cha Elimu Dar Es Salaam (DUCE) na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) ni mshindi wa tatu. Pia kipengele cha pili ni taasisi zilizopo katika ngazi ya tatu ya ukomavu wa TEHAMA Serikalini Halmashauri ya Wilaya ya Geita imekuwa kinara kwa kuwa mshindi wa kwanza, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ikishika nafasi ya pili na nafasi ya tatu ni Halmashauri ya Wilaya ya Kyela.

Katika kundi la pili la taasisi kinara katika kuunganisha na kubadilishana taarifa kupitia Mfumo wa kubadilishana taarifa Serikalini (GoVESB) kipengele cha kwanza cha mtoaji bora wa data kupitia mfumo huo, mshindi ni Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), huku kipengele cha pili, Mtumiaji bora wa data kupitia mfumo huo mshindi ni Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya juu (HESLB).

Aidha, katika kundi hilo kinara wa uwezeshaji mifumo kubadilishana taarifa kupitia GoVESB, Mshindi ni Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS).

Katika kundi la tatu kwa taasisi hodari kwenye Matumizi ya TEHAMA katika kuwashirikisha wananchi mshindi wa kwanza ni Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Dodoma (DUWASA), Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) nafasi ya pili na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa mazingira Mjini Mwanza (MWAUWASA) kushika nafasi ya tatu.

Akizungumza baada ya kupokea tuzo, Mkurugenzi wa DUWASA, Mhandisi Aron Joseph, amesema ni mara ya pili kushinda tuzo hiyo huku akitaja siri ya mafanikio hayo kuwa ni namna wanavyoshirikisha wananchi kwa kutumia mifumo ambayo imetengenezwa na e-GA ikiwamo mfumo wa e-mrejesho ambao wamekuwa wakipokea taarifa na maoni ya wananchi.

**"Kilichotufanya tuwe kinara wa kundi hili ni muda tunaotumia kujibu wananchi waliotoa maoni au taarifa kupitia e-mrejesho, tunapokea taarifa na tunajibu kwa wakati tumejiwekea kujibu ndani ya saa 24 na kama ni suala linalohitaji muda mrefu ili kutoa majibu tumejiwekea muda pia,"**

Naye, Mkuu wa Idara ya Rasilimali watu Halmashauri ya Wilaya ya Geita, Khashim Lugome, amesema ni mara ya pili kushinda na akatoa wito kwa taasisi zingine kuendelea kuweka jitihada ili kupata ushindi wa aina hiyo.

Afisa TEHAMA kutoka HESLB, Moses Mwangene, amesema ushindi wa Bodi hiyo unatokana na ufanisi na namna wanavyoboresha mifumo na kuwezesha ubadilishanaji wa taarifa kati ya taasisi na taasisi. "Hii inatokana na uimara na usalama wa mifumo ya e-GA kutovujisha taarifa," amesema.

Meneja wa Mifumo kutoka NSSF, Mihayo Mathayo, amesema tuzo hiyo inaonesha walivyofanya kazi kwa bidii na kujisahihisha maeneo ambayo walikuwa hawafanyi vizuri na kwasasa wanafanya vizuri kwa kuzingatia sheria, viwango na miongozo.

Mkurugenzi wa TEHAMA, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Erick Kitali, amesema mifumo mingi ya ofisi hiyo inatumika na wananchi na wamekuwa wakizingatia sheria na miongozo inayotolewa ili kuhakikisha taarifa zinasomana.



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb), akimkabidhi Mkurugenzi Mtendaji wa DUWASA Mhandisi Aron joseph Tuzo ya Ushindi wa Taasisi inayoongoza katika kushirikisha wananchi.*




# Utekelezaji Maazimio Kikao Kazi cha Tano Waleta tija Serikali Mtandao

Na. Queenter Mawinda | Afisa Habari Mwandamizi

Katika hatua ya kuunganisha na kurahisisha huduma za Serikali kupitia Mfumo wa Orodha ya Huduma za Serikali (GSD), zaidi ya michakato 900 ya utoaji huduma imeandaliwa na kuingizwa katika mfumo huo kufikia mwezi Februari, mwaka 2026. Wakati huo huo taasisi nyingine zimeendelea kukamilisha utekelezaji wa michakato ya kuorodhesha huduma zao.

kilichofanyika jijini Arusha Februari 2025, yakilenga kuharakisha mageuzi ya kidigitali katika sekta ya umma.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa maazimio hayo wakati wa kufunga kikao hicho, Mhadhiri na Mtafiti kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Dkt. Florence Rashid, amesema Serikali imepiga hatua kubwa katika maeneo kadhaa yaliyokubaliwa na wadau, katika eneo la Serikali Mtandao.

Amesema, kuingizwa kwa huduma hizo katika mfumo wa GSD kunatarajiwa kuongeza uwazi, kurahisisha upatikanaji wa taarifa na kuimarisha ufanisi katika utoaji wa huduma za umma kwa njia za kidigitali.

> **“Kwa kuweka michakato hii katika mfumo mmoja, tunajenga msingi wa uwazi na uwajibikaji, huku tukirahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wananchi,”** amesema.

Katika kuimarisha ubora wa huduma, Dkt. Florence amesema Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imejumuisha katika mpango kazi wake mapitio na maboresho ya Mwongozo wa Uboreshaji wa Michakato ya Kibiashara (Business Process Improvement- BPI).

Amesema mwongozo huo utasaidia kurahisisha na kuoanisha utoaji wa huduma katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, taasisi na mashirika ya umma.

> **“Mwongozo huu utakuwa dira ya pamoja katika kuboresha michakato na kuondoa urasimu usio wa lazima,”** amesema.

Kuhusu azimio la kuwajengea uwezo watumishi wa umma katika eneo la usalama wa mtandao, Dkt. Florence amesema Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) imeendelea kutoa mafunzo ya nadharia na vitendo kwa wataalamu wa TEHAMA katika taasisi za umma.




*Rasi wa Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Ang'avu kutoka chuo kikuu cha Dodoma (UDOM) Dkt.Florence Rashid, akisoma utekelezaji wa maazimio ya kikao kazi cha 5 cha Serikali Mtandao.*

Kwa mujibu wa takwimu zilizowasilishwa, mwaka 2025 wataalamu 135 wa TEHAMA kutoka taasisi 127 walipatiwa mafunzo ya kiufundi, huku taasisi 378 zikifikiwa na mafunzo ya kudhibiti matishio ya kimtandao.

Aidha, wadau walikubaliana kuwa taasisi za umma zitenge rasilimali kuelimisha juu ya usalama wa mtandao kwa watumishi wanaotumia mifumo ya TEHAMA angalau mara moja kwa mwaka, ili kupunguza hatari ya mashambulizi ya kimtandao.

Kuhusu Mfumo wa Majaribio ya Kujipima Mwenyewe, amesema e-GA imebuni mfumo wa Majaribio ya Kujipima Mwenyewe unaojulikana kama 'Online Self-Assessment Test (OSAT)', unaowezesha watumishi kufanya tathmini binafsi ya uelewa wao kuhusu masuala mbalimbali, ikiwemo usalama wa mtandao, na kupata mrejesho papo hapo.

Dkt. Florence amesema majaribio ya awali ya mfumo huo tayari yameanza kwa ushiriki wa taasisi kadhaa, huku maboresho yakitarajiwa kufanyika kabla ya uzinduzi rasmi, hatua inayolenga kuongeza uwajibikaji na uelewa wa watumishi kuhusu matumizi salama ya mifumo ya kidigitali.

Kwa upande wa changamoto ya upatikanaji mdogo wa mifumo ya kidigitali vijijini, amesema Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) inaendelea kupanua miundombinu ya mawasiliano ili kuhakikisha wananchi wengi zaidi wanafikiwa na huduma za mtandao.

Amesema, kukamilika kwa minara 758 ya mawasiliano kunatarajiwa kuongeza kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa mtandao vijijini, na hivyo kupunguza pengo la kidigitali kati ya mijini na vijijini.

Katika hatua nyingine, wadau wamesisitiza umuhimu wa taasisi za umma kujenga uwezo wa kupokea na kutumia teknolojia zinazoibukia katika utoaji wa huduma.

Akizungumzia utekelezaji wake, Dkt. Florence amesema, e-GA kupitia Kituo chake cha Utafiti na Ubunifu wa Serikali Mtandao, imeanza kuunganisha teknolojia mpya katika mifumo mbalimbali ya Serikali ili kuongeza ufanisi.

# Karibuni Viongozi



*Katibu Mkuu Kiongozi Mhe. Balozi Dkt. Mosses Kusiluka (kushoto) akisalimiana na Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Mhandisi Benedict Ndomba (kulia) mara baada ya kuwasili katika viwanja vya AICC Arusha*



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb) (kushoto) akisalimiana na Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Mhandisi Benedict Ndomba (kulia) mara baada ya kuwasili katika viwanja vya AICC Arusha*

# Hotuba na salamu kutoka kwa viongozi



*Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Bw. Xavier Daudi akitoa salamu wakati wa kikao kazi cha 6 cha Serikali Mtandao*



*Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha Dkt. Toba Nguvila akitoa salamu wakati wa kikao kazi cha 6 cha Serikali Mtandao*

# Tuzo za Serikali Mtandao




*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb) (kushoto) akimkabidhi Mkurugenzi wa TEHAMA Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) Bw. Donald Mhaiki, tuzo ya mshindi wa kwanza wa Taasisi inayozingatia Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao katika ukomavu waTEHAMA hatua ya 4 (Level 4 of e-Government Capability Maturity).*



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb), akimkabidhi Mkurugenzi Mtendaji wa DUWASA Mhandisi Aron joseph Tuzo ya mshindi wa kwanza wa Taasisi inayoongoza katika kushirikisha wananchi (Best Performance in Utilization of ICT in Customer Engagement )*

# Tuzo za Serikali Mtandao



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb) (kushoto) akimkabidhi Bw. Mosses Mwangene kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) tuzo ya mshindi wa Taasisi inayotumia Taarifa nyingi (Best Data Consumer) kwenye Mfumo Mkuu wa Ubadilishanaji Taarifa Serikalini (Government Enterprise Service Bus - GOVESB)*



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb) (kushoto) akimkabidhi mwakilishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita Tuzo ya mshindi wa kwanza wa Taasisi inayozingatia Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao katika ukomavu wa TEHAMA hatua ya 3 (Level 3 of e-Government Capability Maturity)*

# Uwasilishaji wa mada na Majadiliano



*Mtendaji Mkuu wa TEHAMA & Mshauri wa Kimataifa kutoka kampuni ya Cybergen Bw. Samvit Rawal akitoa mada wakati wa kikao kazi cha 6 cha Serikali Mtandao.*



Bw. Benjamin Dotto
Mkurugenzi wa Miundombinu na Uendeshaji



Dkt. John M. Sausi
Mkurugenzi wa Mifumo ya Fedha na Huduma za TEHAMA - Wizara ya Fedha



Dkt. Angelina Misso
Mkurugenzi Msaidizi wa Uendelezaji wa Mifumo kutoka Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari

# Uwasilishaji wa mada na Majadiliano




*Meneja Usambazaji kutoka kampuni ya SOPHOS Bw. Rajkumar Popat akitoa wasilisho wakati wa kikao kazi cha 6 cha Serikali Mtandao Jijini Arusha*



Mr. Macrice Daniel Mbodo
Posta Masta Mkuu



Dkt. Fredrick Ishengoma
Mhadhiri Mwandamizi - Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM)

# Uwasilishaji wa mada




Mrakibu wa Polisi Godfrey Kapinga
Afisa Mkuu – Teknolojia ya Habari na Mawasiliano akiwasilisha mada wakati wa kikao kazi cha 6 cha Serikali Mtandao.




Bw. Francis Sanguna
Mkurugenzi wa Huduma za Uwezeshaji - Bodi ya Utalii Tanzania akiwasilisha mada wakati wa kikao kazi cha 6 cha Serikali Mtandao.



*Mkuu wa Kitengo cha Mifumo ya Kidijitali na Mtandao wa vitu kutoka Vodacom Tanzania Bi.Yvone John Bayona akiwasilisha mada wakati wa kikao kazi cha 6 cha Serikali Mtandao.*

# Maonesho




*Katibu Mkuu Kiongozi Mhe. Balozi Dkt. Mosses Kusiluka (kushoto) akisikiliza maelezo kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na uhusiano kwa Umma Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Bw. Rolf Kibaya wakati alipotembelea banda la maonesho la TCRA.*




*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb) (kushoto) akisikiliza maelezo kutoka kwa Afisa TEHAMA wa Mamlaka ya Serikali Mtandao Bw. Francis Mhangwa wakati alipotembelea banda la maonesho la e-GA*

# Maonesho




*Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida, Dkt Fatma Mganga (katikati) akisikiliza maelezo kutoka kwa Mtaalamu wa kampuni ya SOPHOS wakati alipotembelea banda la maonesho la SOPHOS .*




*Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa wa Arusha Bw. Mosses Pesha. (kushoto) akisikiliza maelezo kutoka kwa Watumishi wa Watumishi Housing Investiment (WHI) wakati alipotembelea banda la maonesho la WHI*

# Picha za pamoja




*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb) (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)*




*Katibu Mkuu Kiongozi Mhe. Balozi Dkt. Mosses Kusiluka (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na kamati ya maandalizi ya kikao kazi cha 6 cha Serikali Mtandao.*

# Picha za pamoja



*Katibu Mkuu Kiongozi Mhe. Balozi Dkt. Mosses Kusiluka (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa Dini na viongozi wa Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA).*



*Katibu Mkuu Kiongozi Mhe. Balozi Dkt. Mosses Kusiluka (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Wakuu wa Taasisi na Mashirika ya Umma .*

# Wadhamini




*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb) (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na wadhamini wa kikao kazi cha 6 cha Serikali Mtandao.*



*Katibu Mkuu Kiongozi Mhe. Balozi Dkt. Mosses Kusiluka (kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na wadhamini wa kikao kazi cha 6 cha Serikali Mtandao.*

# Shukrani



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb), (katikati) akipokea tuzo ya shukrani kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi e-GA Dkt. Mussa Kissaka.Tuzo hiyo ni ishara ya kutambua jitihada za Mhe. Waziri katika kukuza Serikali Mtandao.Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa e-GA mhandisi Benedict Ndomba.*




*Katibu Mkuu Kiongozi Mhe. Balozi Dkt. Mosses Kusiluka (kushoto) akipokea tuzo ya shukrani kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi e-GA Dkt. Mussa Kissaka.Tuzo hiyo ni ishara ya kutambua jitihada za Mhe. Balozi katika kukuza Serikali Mtandao.*

6th

e-Gov

Annual Conference 2026

Ofisi ya Rais,
Mamlaka ya Serikali Mtandao,
Mtumba-Mtaa wa Mawasiliano,
S.L.P 2833, 40404 DODOMA.

Barua pepe: barua@ega.go.tz

Simu: +255 026 - 296 1957